# Wahusika wa Kiuhalisiamazingaombwe na Usawiri wa Mivurugo ya Kijamii katika *Babu Alipofufuka* (2001), *Dunia Yao* (2006) na *Bina-Adamu!* (2002)

*Sylvester Kimugung, Magdaline Wafula* na *Peter Simatei*
*Chuo Kikuu cha cha Moi*

**Ikisiri**

**Makala haya yanahakiki wahusika wa kiuhalisiamazingaombwe na namna wanavyowasilisha mivurugo ya jamii katika riwaya za *Babu Alipofufuka* (2001) na *Dunia Yao* (2006) za Said Ahmed Mohamed, na *Bina-Adamu!* (2001) ya Kyallo Wamitila. Makala yalibaini kuwa wahusika wa kiuhalisiamazingaombwe wanatumia njia zisizo za kisayansi wala urazini kusafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine na kuwasiliana baina yao. Aidha, wahusika wana nguvu za kimazingaombwe zinazowafanya kufanya kazi mbalimbali kwa urahisi. Kwa ujumla, wahusika wana sifa za kimazingaombwe zinazokaidi kaida za Aristotle na Plato. Makala haya ni muhimu kkatika kuelewa matumizi ya mitindo ya uhalisiamazingaombwe na namna inavyowasilisha mivurugo ya jamii.**

**Maneno Muhimu:** Wahusika, Uhalisiamazingaombwe, Uswawiri, Jamii

## Utangulizi na Mapitio ya Maandishi

Kwa mujibu wa Kegley na Raymond (2014) jamii ya kisasa imepitia mabadiliko mengi sana ikilinganishwa na jamii ya hapo awali. Ban Kimoon (aliyekuwa sekretari Shirika la Umoja la Kimataifa) alisema katika kongamano la Shirika la Umoja la Mataifa katika Chuo Kikuu cha Luxemboung mwaka wa 2012 kuwa tunaishi katika dunia hatari kwa maisha ya binadamu. Kuna kuzoroteka kwa uchumi, ukaidi, hewa chafu, uhaba wa raslimali na maenezi ya magonjwa hatari duniani. Mathalan, ugonjwa wa *Covid-19* ulioanzia Wuhan, China Disemba 2019 na ambao umesambaa kote duniani na kuuwa watu zaidi ya 18,939 na wengine zaidi ya 424,830 kuambukizwa[1]. Kwa hivyo mitindo ya uhalisia iliyokuwa ikitumiwa kuelezea jamii imepitwa na wakati. Uhalisia ulikuwa unatumiwa na waandishi kuakisi jinsi mambo yalivyo katika jamii. Yaani, fasihi lazima iakisi hali halisi ya maisha katika jamii inayohusika (Wafula na Njogu, 2007). Kutokana na mabadiliko

[1] Taarifa hii ni kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani kutoka tovuti yao https://www.who.ac.ke tarehe 25/3/2020 saa 11.42 asubuhi. Ugonjwa huu ulianzia nchini China na kusambaa kote duniani. Hivi sasa nchi ya Italia inaongoza kwa idadi ya vifo 6,820. Ugonjwa huu umefanya nchi nyingi kusimamisha shughuli zao na watu kusalia nyumbani hivyo basi umesambaratisha uchumi.

ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kisayansi, kiteknolojia na kisanaa mitindo ya uhalisia ilifika kilele chake katika Kipindi cha Mapinduzi ya Viwanda na maendeleo mengine ya Kisayansi na hivyo basi kukosa kukidhi mahitaji ya wananchi (Mrikaria 2009). Mwamzandi (2013) anasisitiza mabadiliko hayo kwa kusema kuwa sanaa huenda na wakati na mahitaji ya binadamu. Uhalisia ulifaa katika kipindi fulani cha uandishi kuliko uandishi wa aina yoyote na ilipodhihiri kwamba uhalisia hungeweza kushughulikia dhamira za kisasa, basi ilibidi nao utupiliwe mbali kama kinavyotarajia kipindi cha hivi leo. Hii imepelekea waandishi wa fasihi kukiuka uhalisia na kutafuta njia mbadala ya kuwasilisha fasihi. Ni njia hii mbadala ndio tunayoita uhalisiamazingaombwe. Mtindo mmojawapo wa uhalisiamazingaombwe ni matumizi ya wahusika wa uhalisimazingaombwe.

Riwaya za hapo awali zilikuwa zikitumia wahusika wa kihalisia. Wahusika wa kihalisia ni wahusika ambao wanafuata kaida za Aristotle na Plato kuhusu sifa za wahusika. Sifa hizo ni: wahusika kuwa na sifa sawia na binadamu wa kawaida, ufaafu, uhalisia na mfanano kuanzia mwanzo wa kazi za fasihi hadi mwisho. Katika Riwaya za Kimazingaombwe wahusika wa kihalisia walikaidiwa na wahusika kuchukua sifa za kimazingaombwe. Kwa mujibu wa Khamis (2008), riwaya za Kiswahili zilianza kuchukua mwelekeo tofauti kuanzia mwaka wa 1990 na kukaidi kaida za Aristotle na Plato. Riwaya zinazotumia mitindo ya uhalisiamazingaombwe zilianza kutumika. Riwaya za kimazingaombwe wahusika wengi ni vivuli vya watu au ni dhana zinazopewa uhai ili kusimamia kwa matendo dhamira, hoja, mitazamo na falsafa ya mwandishi. Ingawa ni wahusika ambao wanasadikika kimantiki. Baadhi ni vizuu au maiti wanaofufuka. Wengine ni mitume wanaorudi tena duniani. Wengine ni watu wa miujiza tu wanaoishi karne kwa karne bila ya kufa wala kuzeeka. Ni watu wenye uwezo wa kuisukuma milima. Wenye uwezo wa kupenya na kuishi ardhini na majini. Wenye uwezo wa kumeza mito ya maji matumboni mwao ili kwenda kuyamwaga pahala pengine. Kuna wengine wanaochorwa kwa sifa za kiungu. Pengine ni wahusika wa jinsi mbalimbali wanaowekwa pahala pamoja kwa haja ya mwandishi kuelezea dhana fulani ya kusisitiza ile dhamira ya umataifa: Wazungu, Waafrika, Waarabu, Wahindi na Wajapani. Mtafiti anakubaliana na maelezo hayo ya Khamis kuwa masuala ya kijamii yamebadilika na kuwa wahusika wa kihalisia hawataweza kuelezea masuala hayo kwa njia ipasavyo. Hivyo basi, waandishi wa riwaya teule wametumia wahusika wa kimazingaombwe ili kusawiri mivurugo ya jamii ya kisasa. Katika makala haya, mtafiti amejadili wahusika hawa wa kimazingaombwe na kuonyesha wanavyofanikishwa usawiri wa mivurugo ya jamii ya kisasa.

Makala haya yameongozwa na Nadharia ya Uhalisiamazingaombwe iliyoasisiwa na Franz Roh (1925) na kuhakikiwa na wanafalsafa wengine wa fasihi kama Warnes (2009). Dhana ya uhalisaimazingaombwe ilibuniwa na Mjerumani Franz Roh mwaka wa 1925 alipokuwa akirejelea mtindo wa upakaji rangi na kuifahamika zaidi kutokana na maandishi ya Gabriel Garcia Marquez's *One Hunderd Years of Solitude (1967).* Ilibuniwa baada ya Vita vya Kwanza vya dunia katika bara la

Uropa. Baadaye iliendelezwa katika bara la Marekani kusini. Dhana hii ilibuniwa kukaidi kaida za uhalisiafifi, uhalisia nafsi, na uhalisia. Kwa sababu Roh alikuwa anarejelea upagaji rangi katika ufafanuzi wake; makala haya yametumia ufafanuzi wa Warnes (2009) ili kujenga mwenga wa nadharia ambao umetumika katika uchanganuzi wa data. Warnes (2009) anajadili mhimili wa Nadharia ya Uhalisiamazingaombwe: upingaji wa dhana uhalisia, usayansi na urazini za kimagharibi (irreverence). Warnes anaonyesha upungufu wa dhana hizi za kimagharibi. Dhana hizi ni za kipindi cha usasa na zimekuwa kandamifu kwa maisha ya binadamu hivyo basi kutiwa shuku katika kazi za fasihi ili kuporomosha. Lengo ni kuonyesha jinsi dhana hizi zimekuwa kandamifu kwa maisha ya binadamu kinyume na matarajio yake. Warnes ametuonyesha wataalamu wawili waliotumia Nadharia ya Uhalisiamazingaombwe: Jorge Luis Borges na Salma Rushdie. Borges alidengua matumizi ya uhalisia, urazini na usayansi. Japo Borges hakuwa ameegemea matumizi ya uhalisiamazingaombwe; maoni yake yalitia hamu waandishi wa baadaye kupinga dhana za kimagharibi. Borges katika tahakiki mojawapo ya Kijerumani itwayo *Turkish Tales (1926)* alisema kuwa riwaya za kimazingaombwe zinasawiri mazingaombwe kama yanatukia kihalisia. Mathalan, malaika wako duniani jinsi miti ilivyo. Japo uhalisia upo, huwezi kuthibitishwa moja kwa moja; huwa tunafafanua tu![2] Aidha, Salma Rushdie katika riwaya yake ya *Satanic Verses (1988)* alibuni wahusika wanaopeperuka kutoka bara la India hadi Britania, wanaokaidi nguvu za ardhi (*gravity),* wanaogeuka kuwa shetani au wanyama, mtoto ambaye alizaliwa na mama watatu, mwanaume aliyekuwa akizeeka maradufu na mwanamke aliye na ngozi ya kioo. Sifa hizi zinapinga kaida uhalisia, usayansi na urazini za kimagharibi. Kwa hivyo katika makala haya tumeonyesha jinsi riwaya teule zinavyoonyesha sifa hizi kupitia wahusika wa kiuhalisiamazingaombwe.

**Sifa za Wahusika wa Kiuhalisiamazingaombwe na Usawiri wa Mivurugo ya Kijamii**

Katika sehemu hii, sifa tatu za wahusika katika riwaya teule zimehakikiwa na kuonyesha mivurugo ya jamii inavyosawiriwa.

**Wahusika wenye Nafsi Mbili**

Mhusika mwenye nafsi mbili ni mhusika ambaye ni mmoja lakini amechukua mwelekeo tofauti ili kuwasilisha dhamira fulani. Mathalan, mhusika mmoja amegawika kuwa wahusika wawili. Kwa hivyo, wahusika hawa wanawasiliana ndani ya huyu mhusika moja. Wakati mwingine ni mhusika moja lakini amechukua viwango tofauti vya uhusika. Hii inakaidi kaida za Aristotle kuwa mhusika anafaa kuwa anabainika tangia mwanzo, mhusika mmoja hafai kugawika au hata kubadilika (Tilak 1993).

[2] Maelezo kama haya yanatolewa na Waliula (2010) akimnukuu (Simpkin, 1988). Uhalisia huwezi kuelezwa kikamilifu kwa sababu umefungama na minyororo ya lugha.

Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (*BAF*)*,* K ni mhusika mwenye nafsi mbili. Anabadilishwa kutoka nafsi ya uhalisia na kuingizwa ulimwengu wa uhalisiamazingaombwe ili aweze kuona changamoto raia wanapitia kijijini mwake. Hii ni kwa sababu akiwa katika nafsi ya kihalisia haoni changamoto hizo. Uhalisia umekuwa dhana za kipindi cha sasa ambazo ni kandamifu katika maisha ya binadamu (Rettova 2016). Hivyo basi, uhalisiamazingaombwe unadengua hali hii kupitia mhusika K. Udenguzi wa uhalisia unatokea pale K anapolazimishwa kuvaa figu la sura ya mchwa, kisha kujiua kwa kujikaba roho, kuanguka chini na kufa. Anaguswa na Mzuka na kugeuka mchwa na anapata uwezo wa kupitia chini kwenye mizizi ya gugu la ukoko. Baadaye anapata uwezo wa kupaa hewani na kutua kama ndege (*BAF* 82). Katika nafsi ya kihalisia K ni mbinafsi na hapendi kuhusishwa na umaskini na hivyo anavaa figu hivi kwamba hata Mussa rafiki wa utotoni hamtambui. Wananchi kutoka mazingira alimolelewa wanambandika jina la 'Protausi' kumaanisha kuwa anapaswa kuwalinda na kuwahudumia raia lakini amejitwika uwezo wa mali ya kujinufaisha yeye binafsi (*BAF*, 86). K akiwa kiongozi alikuwa amejitenga na raia wake:

1. K alitoa miwani yake ya kuziba macho. Haraka aliivaa. Makusudi hakutaka kuona mandhari yoyote nje. Na'yeye alihifadhika asionekane na wale waliokuwa *wakiutwanga nje.* Ulikuwa utamaduni wa kujificha katika kila kitu alichokifanya, na kila pahala alipokuwa au alikokwenda. (*BAF*, 18)

Nafsi ya uhalisia ya K, ilimruhusu yeye kujitenga na raia ambao walikuwa wamemchagua ili kuwahudumia. Raia wake wanapata changamoto mbalimbali kutokana na ukosefu wa uongozi bora. Ni kutokana na kuwa na nafsi ya pili (nafsi ya uhalisiamazingaombwe), iliyovaa figu, ndipo anaona maangaiko ya raia wake. K akiwa katika hali ya figu anaonyeshwa jinsi raia wanavyoteseka katika usafiri wa umma:

2. Gari lilikuwa limejaa. Watu pachapacha. Lakini nafasi ya kujibana mtu mmoja ilikuwepo, iwapo watu fulani wangejitolea kushuka kabla ya kufika kituo cha polisi na kutangulia mbele kulingojea gari litakapokwisha *kupek'sheniwa.* (*BAF*, 133)

K anaonyeshwa jinsi raia wake wamekuwa wakiteseka katika usafiri wa umma. Hakuna magari ya kutosha. Magari ambayo yako yana dosari chungu nzima. Polisi hawafanyi kazi zao. Wanachukua hongo barabarani. Hata gari likiwa limejaa linaruhusiwa kuendelea na safari. Matokeo ni ajali barabarani zinazosababisha mauti. Neno *kupek'sheniwa* limetumiwa na mwandishi kiatiliki kwa makusudi maalumu. Kwanza, kazi za kiuhalisimazingaombwe zinavuruga maandishi ili kusawiri hali halisia ya mivurugo ya jamii (Childs na Fowler, 2006). Mivurugo inayojitokeza katika ibara hii ni polisi kukagua magari tu kama desturi na iwapo gari lina dosari, hawachukui hatua zozote. Kinyume wanachukua hongo. Matokeo yake ni kuwa usalama barabarani unazoroteka na ajali kushamiri.

Katika riwaya ya *Dunia Yao* (*DY*)*,* mhusika mkuu amechukua nafsi mbili: Ndi- na –Ye. Mhusika huyu anakisiwa alikuwa anaitwa Ndiye wakati alipozaliwa na alipoajiriwa katika ofisi ya serikali. Katika muktadha wa Nadharia ya Uhalisamazingaombwe, Ndiye alikuwa mhusika wa kihalisia. Katika hali hii mhusika huyu angeweza kuona mivurugo katika jamii yake. Hii inabainika katika ukurasa wa 5, baada ya Ndiye kumaliza digrii yake alifanya kazi mbalimbali serikalini kama kuwa mwalimu katika shule za sekondari, na ukarani. Akiwa katika hali hii ya uhalisia hakuona ufisadi uliokuwa umekithiri katika ofisi yake:

3. Baada ya mageuzi, kazi za ngazi za juu zilitengwa kwa wastahiki fulani na wala hazikutegemea kuwa na elimu, akili au busara. Muhimu zaidi wewe ulikuwa nani, mtoto au mjukuu wa bwana gani na kama unaitikia 'ndiyo' kila wakati. (*DY*, 16)

Neno mageuzi hapa linamaanisha wakati ambapo nchi husika ilipojipatia uhuru kutoka kwa wakoloni. Ilitarajiwa kuwa baada ya nchi kujikwamua kutoka minyororo ya ukoloni, maisha yangeboreka. Hata hivyo, waafrika viongozi walianza kuwadhulumu na kuwanyanyasa wenzao. Walianza kuendeleza ufisadi katika nyanja mbalimbali za serikalini. Mojawapo ikiwa ofisi alipokuwa akifanya kazi Ndiye. Katika hali ya uhalisia, Ndiye angeweza kuuona ufisadi huo. Kwa maneno yake mwenyewe anasema kuwa 'tokea mwanzo sikushughulika na harakati zozote' (*DY*, 16). Wakati ambapo Ndiye alianza kuchukua nafsi ya mbili (nafsi ya uhalisiamazingaombwe) ndipo mivurugo inayoendelea ofisini mwake ikaanza kubainika. Safari ya Ndiye kutoka nafsi ya uhalisia hadi nafsi ya mbili, Ndi- na –Ye, nafsi za uhalisiamazingaombwe ilitukia kupitia usaili wa masuala ya jamii:

4. Kwa nini, kwa mfano, mtu asiweze kukataa jambo asilolitaka? Kwa nini mtu asiwe na maoni huru juu ya mwenendo wa maisha yake na maisha ya walio karibu naye? Kwa nini mtu mwingine awe na haki ya kuharibu maisha yangu na ukoo wangu? Kwa nini mimi niwe kila siku mwenye hatia? Kwa nini mimi tu ndiye niwe mwendawazimu? […] kwa nini nisiwe na haki ya kumweleza mwingine kwa maslahi yangu na yake? Kumweleza jinsi maisha yetu yalivyoangamizwa na mazingira yetu kufanywa machafu na yenye udhia na hatari? (*DY*, 17)

Baada ya Ndiye kuona mivurugo mingi iliyokuwa katika jamii anajiuliza ikiwa mtu anaweza kuzuia. Anashangaa ni kitu kipi kinamfanya mtu kuwakandamiza wengine. Aidha, anashangaa watu hawaoni mivurugo iliyo katika jamii. Watu wengi kuangamia kutokana na matendo maovu ya wengine. Ikumbukwe kwamba nchi ya Ndiye ilikuwa imepata uhuru miaka 42 iliyopita ilhali nchi ilikuwa imezoroteka kiuchumi, kisiasa na kijamii. Ni kutokana na sababu hizi Ndiye alijifungia kwa nyumba na kuwa mnyamavu na jozini:

5. Wazungumzaji wangu wote wa nyama-na-mifupa nimewapoteza. Umebaki utupu wa mambo. Tuko wawili kama mboni za macho-pofu au chongo ingawaje. Ndi- ni mimi na –Ye ni yeye. Mara nyingine –Ye mimi humwita Shaib, […]. Alikuwemo ndani ya nafsi yangu

nilipozaliwa. Miaka iliposonga amemung'unyuka na kusimama mbali kidogo nami. Unaona! Hata majina yetu yamebutuka! (*DY*, 2)

Katika dondoo hili nafsi ya Ndiye iligawika mara mbili; Ndi- na –Ye. Aliamua kujiongelesha peke yake baada ya kukosa watu ambao wangeelewana naye, hata mkewe –Bi M- angeelewana na yeye. Kuashiria uwili, uchangamano, utengano wa kiutu, na vivile kusambaratika kwa utambulisho, ambapo si dhahiri sana kubaini kama Ndi- anayeweza kuwa Ndimi tu au ni Ndiye. Haya yanadhihirisha zaidi katika ibara hii:

6. Tulikuwa peke yetu. Mimi na Shaib. Ndiye mtu pekee niliyeweza kuzungumza naye hapa. […]. Siku hizi sisemi na mtu ila na kivuli cha Shaib. Ye-, yaani Shaib, huzungumza nami ingawa simwoni. […]. Vifo vya makusudi na vya mapuuza. Wizi, ufisadi uliokithiri na utandawazi. (*DY,* 40)

Mazungumzo baina ya Ndi- na –Ye yanatendeka kichwani mwake. Mazungumzo hayo yanabainisha changamoto zinazokumba binadamu. Katika dondoo hili uhalisiamazingaombwe unatumiwa kama nuru ya kumulika mivurugo katika jamii. Mivurugo ambayo hayawezi kuonekana kihalisia. Baadhi ya mivurugo hiyo ni uwizi, uporaji wa mali ya umma, ufisadi katika ofisi za serikali, unyanyasaji na ukandamizaji, mauaji, na maenezi ya utandawazi.

Katika riwaya ya *Bina-Adamu* (*BA*)*,* nafsi ya uhalisia inajitokeza wakati ambapo Binadamu alipozaliwa katika kijiji chake:

7. Nilipozaliwa nilikuta watu wakikiogopa kiini cha kijiji chetu na mpaka leo hii unapoisoma hadithi hii bado wanakiogopa. (*BA*, 7)

Ni katika hali hii ya uhalisia ndipo wanakijiji wanakiogopa kiini cha kijiji. Wanaishi pembezoni na hivyo basi kuteseka. Yeyote angeanza kutafuta kiini cha kijiji akiwa katika hali halisia angepata pingamizi sana:

8. Pale kijijini pana vituko; ukienda kwenye kiini chake utaishia kupatwa na madhara makubwa. Mwanamume atakayeenda huko anaweza kushtukia amebadilika jinsia na kuwa mwanamke kwa kuwa lazima alizunguke jabali kubwa lililoko hapo. (*BA*, 9)

Iwapo Binadamu angesafiri kihalisia katika sehemu hii angebadilika jinsia. Hivyo basi, ilibidi Binadamu abadilishe nafsi yake ya uhalisa hadi uhalisiamazingaombwe ili aweze kuzuru dunia nzima kutafuta changamoto zinazokumba jamii. Katika kubadilisha nafsi yake aliweza kutagusana na viumbe mbalimbali: mazimwi, viunzi vya binadamu, na nyoka. Aidha, alikuwa na uwezo wa kusikia sauti za kimazingaombwe, nguvu za kimazingaombwe kama uwezo wa kuelea juu ya maji, kuwasiliana na waliofariki na hata kuishi kwa miaka na mikaka. Ni kupitia nafsi ya uhalisiamazingaombwe ndiyo Binadamu anatusawiria changamoto zinazokumba nchi zinazoendelea. Mojawapo ya changamoto inayokumba nchi hizi ni uongozi mbaya. Viongozi wanapochaguliwa, mahitaji yao

yanakuwa ya muhimu sana. Katika riwaya ya *BA* tunaambiwa kuwa wao ni kukaa paani na kuchumia matunda (*BA*, 67). Neno matunda limetumiwa kijazanda kumaanisha raslimali ya nchi. Kwa mujibu Poncian na Mgaya (2015) nchi nyingi katika bara la Afrika zimebarikiwa na raslimali. Changamoto iliyopo ni viongozi kutumia ili kuwafaidi raia. Viongozi ndio wamepewa jukumu la kugawa raslimali hizo. Linalobainika ni kuwa wao ndio wanaojigawia kwanza. Wanapata elimu bora, matibabu ya hali ya juu, na barabara nzuri. Lakini raia waliowachagua wanateseka.

Sehemu hii imebainisha kuwa uhusika wa nafsi mbili unamwezesha mwandishi kudengua changamoto zinazokumba jamii ya kisasa. Wahusika wa kihalisia wamekuwa kandamifu, fisadi na wanyanyasaji. Hivyo basi, waandishi wa riwaya za kiuhalisiamazingaombwe wamepiga hatua mbele kwa kubuni wahusika wa kiuhalisiamazingaombwe ambao wanakuwa wakombozi wa changamoto zinazokumba jamii. Aidha, wanasawiri mivurugo ya jamii ya kisasa kama umaskini, uongozi mbaya, utabaka na ukosefu wa ajira.

**Wahusika wenye Uwezo wa Kupaa Angani**

Kwa mujibu wa TUKI (2004) kupaa ni ruka angani, enda juu. Kisayansi hakuna binadamu anayeweza kupaa angani isipokuwa vyombo vinavyoundwa na binadamu kama ndege na aeroplani. Hata hivyo kwa mujibu wa visasili vya Kigiriki, inaaminika Drakula na mwanawe Icarus waliweza kujiundia mabawa na kuwa binadamu wa kwanza kupaa angani. Kwa hivyo kupaa angani ni mojawapo ya vitendo vya kimazingaombwe vilivyotumiwa na waandishi wa riwaya za kimazingaombwe kusawiria mivurugo ya jamii. Katika riwaya ya *BA,* Binadamu anapotagusana na Mwanasayansi, Mhubiri na mwanafalsafa. Mwanasayansi anapaa angani ili kwenda kuangalia *dolly* iliyokuwa imekufa (*BA*, 121). Mwanasayansi anapaa angani kuonyesha kuwa sayansi sio kila kitu na hii inadhihirika pale *dolly* inakufa. Hii ni kuonyesha kuwa sayansi haiwezi kusuluhisha kila kitu; mwanasayansi huyu anakosa kutagusana na Binadamu kuonyesha kuwa mtazamo wa Kimagharibi ni kandamifu kwa maisha. Hivyo basi tunahitaji mtindo wa uhalisimazingaombwe kama kupaa angani ili kufafanua changamoto zinazokumba nchi zinazoendelea (Chanady, 1985).

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* wahusika Ndi- na Bi Mize walikuwa na uwezo wa kupaa angani:

9. Kwamba sasa ananipeleka kwenye bustani zake. Na kweli. Nilianza kuhisi sikanyagi ardhini. Ninaning'inia hewani kwa ureda. Hakika si ndoto. Nilihisi hivyo ingawa sikutambua kama nikitembea au kuruka. (*DY,* 62)

Katika dondoo hili wahusika hawa wanapaa angani ili kuelekea sehemu moja hadi nyingine. Wanapopaa angani wanatueleza uharibifu wa mazingira uliopo katika jamii. Uozo huu unajitokeza Ndi- alipoonyeshwa bustani hii:

10. Nilifumbua macho. Na hapohapo niliyakodoa kwa mshangao. […]. Miti na mimea yote imekauka. Ukavu wa kila pahala. Ukavu wa kijiti

> kudata ukionyesha kidole tu. Miti na mimea inasimama mamia ya maguu ya mashina ya kijivujivu. (*DY*, 62)

Katika dondoo hili uchafuzi wa mazingira unajitokeza kwa upande mkubwa. Kwa mujibu wa Kegley na Raymond (2014) uchafuzi wa mazingira ni suala ibuka katika K21. Uchafuzi wa mazingira umesababisha maji ya bahari kupanda juu ya mwambao wa pwani kutokana na kuyeyuka kwa barafu zilizopo maeneo ya Kusini na Kaskazini ya dunia. Hii inatokana na kuongezeka kwa joto duniani. Hii itahatarisha maisha ya watu zaidi ya milioni 100 wanaoishi mwambao wa pwani. Uchafuzi huu utaathiri maisha ya binadamu duniani. Binadamu wanafaa kuwa waangalifu ili kukabiliana na athari hizi.

Mwishoni wa riwaya ya *DY,* tunaambiwa kuwa Ndi- aliruka angani:

11. Baada ya kuwasimulia hadithi yangu, nilijikuta ninavutwa kuruka na kuleleja hewani kama kwembe juu ya bahari ya Hindi. Na huko nikatuwama kutazama upeo wa macho kwenye dunia yao. Kaskasini kusini mashariki na magharibi […] Magharibi ya kaskazini, niliwashuhudia watu waliojipweteka juu ya *morischea*, wanakula raha za maendeleo yaliyokuwa yakitekenya zaidi na teknolojia, hasa ile ya *high tech* na mawasiliano ya *digital*; […]. Lakini kusini na mashariki niliona watu duni wakitimuka timtim, mbio, hemkahemka, wanacheza ngoma tu …na hofu, na kukata tamaa, wasiwasi, woga na mchukuo wa kinyama …huyu kakamata rungu. Mwingine ana panga. Yule kashika kigongo na mwenzake kainua mrau …maneno. Kutukanana. Kusimbuliana. Kulana roho. Kuangamizana. Mradi ugomvi. Fujo na vita vya wenyewe kwa wenyewe visivyokwisha. (*DY*, 212)

Katika dondoo hili dunia ya kisasa imegawika sehemu mbili. Nchi zinazoishi katika sehemu za Kusini Mashariki zinazojulikana kama *Global South* ambazo zina changamoto nyingi sana. Zinajulikana kama maeneo hatari. Katika sehemu hii kuna umaskini, vita na udikteta. Japo demokrasia ziliingia nchi hizi kuanzia mwaka wa 1980, serikali hazijiendelezi kidemokrasia ipasavyo. Mara nyingi kunao vita baada ya uchaguzi na ukeugaji wa haki za binadamu. Tofauti na nchi za Kaskazini Magharibi zinazojulikana kama *Global North.* Nchi hizi tofauti na *Global South* zimeimarika. Zina amani, demokrasia ni ya juu, miundo misingi na teknolojia imesambaa kote na ni ya hali ya juu.

Katika riwaya ya *BAF,* K anageuka hewa na kupaa angani:

12. Lakini alikuwa akipotea mbele ya macho yao. Kidawa na Bamkubwa na hata Yule mwanamke kichaa Kikuba walikuwa wakikodoa macho kwa mshangao kumtazama alivyokuwa akigeuka hewa na kupaa. (*BAF*, 168)

Tukio hili linatukia baada ya K kukutana na watoto wake Kidawa, Bamkumbwa na bibiye Kidawa. Ikumbukwe kuwa familia ya K ilisambaratika kutokana na K

kuhepa majukumu ya familia yake. Katika muktadha huu, K kubadilika hewa na kupaa angani ni ishara kuwa familia yoyote haiwezi kujengwa kwa kuhepa majukumu. Lazima wanandoa wajukumuke katika familia. Kuashiria dhiki ambazo Kidawa na Bamkubwa walikuwa wamepitishwa na baba yao K.

Katika riwaya ya *BAF,* Delpiero ni rafiki mpya wa K, baada ya kupata mamlaka. Ni fisadi kwani ananyakua eneo zima la ardhi la pahali fulani. Anatetewa na K baada ya wavuvi kulalamika kuhusu unyakuzi wa ardhi. Anasemekana ni mhusika wa kiajabu, kwani wavuvi wanahadithia kuwa walimwona akitoa mabawa na kuruka, akitokomea pahala fulani na kisha kurudi na kuondosha magunia ya unga. Hii inamaanisha kuwa ni mlanguzi wa dawa za kulevya. Mara anageuka mweupe badala ya rangi yake ya zeruzeru:

13. Nini hasa Delpiero anafanya hasa haikujulikana, ila wavuvi waliomwona wanahadithia kwamba walimshuhudia mara kadha akiota mbawa na kuruka, […] na kisha kurudi na kudodosha magunia yaliyojaa unga. Amefanya hivyo mara nyingi kwa hakika, hadi yeye mwenyewe amekuwa akigeuka mweupe badala ya rangi yake ya zeruzeru. (*BAF*, 13)

Inaashiria unyama ambao Delpiero alikuwa akitendea watu maishani mwao. Alikuwa akiuza dawa za kulevya. Kupaa angani katika muktadha huu ni kuvunja sheria zilizowekwa nchini na uongozi wa K. Lakini anapovunja sheria hahukumiwi. Kuna utepetevu katika utekelezaji wa sheria na hii imepelekea uovu kuendelea katika jamii ya K.

Katika kilabu cha ***Neo-Casino*** K anaonekana akipeperuka:

14. K alipeperuka kwa mapozi na fahari huku akilazimisha kicheko. Kama wangekuwa watambuzi hata hivyo, wangemwona hakuwa kafwatana na uchangamfu wake wa desturi. Uso wake kwa kweli, ulikuwa umeota mabaka ya wasiwasi na macho yake yamekodoka na kutunga mbele kutazama kitu kisichoonekana na wengine. (*BAF*, 29-30)

K alipokuwa akija katika ***Neo-Casino*** alikuwa akisindikizwa na marafiki wake Di Livio, Delpiero, Miyazawa, na Von Heim. Eneo la ***Neo-Casino*** ni eneo la burudani lisilofikiwa na raia wake. Kila mara K alikuwa anayakwepa majukumu yake na kuja sehemu hii kujivinjari na marafiki zake. Kupeperuka katika dondoo hili ni sawia na kuyakwepa majukumu yake ya kimsingi. Majukumu yake yanafaa kutekelezwa katika eneo lake analowakilisha lakini yeye anakwepa na kukuja kwenye ***Neo-Casino.*** Haya yanathibitika katika dondoo hili:

15. Akili zikazunguka na kuduru. Akili ziliruka na kutua. Walioota manyoya waliota. Kama mazimwi! Walioota mbawa waliota kama tai. Kumbukizi zikenda nyuma na ndoto zikawarusha mbele. Nyuma mafanikio na mashindikano na mbele kutomasa, kushinda na kushindwa pia. Hatimaye bila ya wazo lile la FKK kuparaganyika, Di Livio alijitokeza tena baada ya kutua ardhini. (*BAF*, 46)

Ishara ya mipangilio ya viongozi isiyo na mashiko. Viongozi hawa wameamua kuanza mradi wa FKK ambao ni kilabu cha kueneza ukahaba na uasherati mijini. Hizi ni tamaduni mpya ambazo zinaendeleza uozo katika jamii. Tofauti na mahitaji ya raia anaowakilisha K. Raia wake wanakosa vyakula (*BAF*, 161), na barabara zao ni mbaya (*BAF*, 170). Japo viongozi wanapeperuka na kuwakwepa raia, kupitia mtindo wa kimazingaombwe viongozi hawa wanapatikana pale mzuka anawafuata hadi sehemu hiyo tengwa:

16. Yule mfu alikuja kuning'inia juu ya meza kwa mtindo wa jini la Sinbad; kama mpando wa mshoroba mkubwa wa moshi mweupe mbele ya ajabu na mwemeo wa kila mtu hapo, K aliketi macho juu na kusema nalo hilo dubwana lenye mwili wa moshi na uso wa bango usio macho, nyusi, kope, pua wala mdomo-ila labda masikio yaliyoning'inia pembeni kama tojo za mgomba. (*BAF*, 35)

Kuninginia kwa mfu huyu ni ishara ya kushindwa kwa maovu ambayo yalikuwa yakiendelezwa na kiongozi K bila kujulikana na raia. Wahusika hawa walikuwa wamejificha kutoonekana na raia. Umuhimu wa mtindo wa uhalisiamazingaombwe wa kubuni mhusika ambaye ananing'inia imetuwezesha kupatana na viongozi hao kandamifu na wanaojificha. Inavyoonekana K alibidi kuzungumza na mfu huyu. Ni kupitia mtindo huu wa uhalisiamazingaombwe ndipo maovu yatendwayo na K yanaweza kusawiriwa na riwaya za Kiswahili za kimazingaombwe.

Kwa ujumla wahusika wanaopaa angani wametumiwa na waandishi wa riwaya teule ili kusawiri maovu yanayotukia duniani. Katika kufanya hivyo, ufinyo wa wakati na mahali wa wahusika wa kihalisia ulisuluhishwa. Wahusika hawa wa kiuhalisiamazingaombwe ni mwafaka katika dunia ya kisasa ambayo utandawazi umefanya dunia kuwa kijiji. Wahusika hawa wameweza kuelezea moja kwa moja mivurugo inayokumba dunia nzima kutokana na uwezo wao wa kupaa angani na kusafiri masafa marefu bila vizuizi ambavyo vingekumba wahusika wa kihalisia.

**Wahusika wenye Sifa Zisizo za Kawaida**

Kwa mujibu wa Plato na Aristotle, wahusika wa fasihi wanafaa kuwa na sifa za kihalisia. Sifa ambazo zinaweza kutekelezwa na binadamu waliomo duniani. Hata hivyo, katika riwaya za kimazingaombwe kuna wahusika wengi ambao wana sifa zisizo za kawaida. Katika riwaya ya *BA,* Hanna alikuwa ni binadamu aliyekuwa akimwongoza Binadamu katika safari yake ya kutafuta kiini cha jamii yake. Alimwongoza yeye katika sehemu mbalimbali na kudhihirisha sifa zifuatazo za kimazingaombwe: Aliweza kukonyeza mwangaza. Kukonyeza mwangaza ni kumulika kama vile tochi au stima. Sifa hii imekuwa ya kimazingaombwe kwa sababu binadamu halisia hawezi kukonyeza mwangaza. Binadamu aliweza kumtambua Hanna kutokana na mwangaza uliokuwa ukikonyeza kwenye kisogo chake kama wa kimulimuli (*BA*, 25). Fauka ya hayo, mikono yake ikiakisi mwanga mkali na hata kumetameta kama ngozi ya nyoka (*BA*, 30). Jambo hili linadhihirisha

ukosefu wa uthabiti wa wahusika. Aidha, Hanna aliweza kutembea majini bila kuzama:

17. Sasa tulishika njia na kuingia kwenye sehemu iliyokuwa na bwawa kubwa. Katikati palikuwa na kisiwa kikubwa sana. Hanna alitangulia hadi alipofika karibu na ukingo wa lile bwawa kisha nikamwona anajitosa majini na kuendelea na safari yake huku akinipungia mkono. (*BA*, 44)

Hapa, Hanna alikuwa na uwezo wa kutembea juu ya maji bila kuzama. Hili ni tukio la kimazingaombwe ambalo haliwezi kutendwa na wahusika halisia. Fauka ya hayo, Binadamu ni mhusika mwengine ambaye hakuzama majini. Binadamu alipokuwa akisafiri alikutana na maji yaliyokuwa yametulia ajabu. Ghafla maji hayo yalianza kwenda kasi ya ajabu. Binadamu aliingia ndani yake ili kuwafuata waongozi wake. Maajabu Binadamu hakuzama. Nilishangaa kuwa mara hii niliweza kuushikilia ule mkongojo pamoja na mkoba wangu ambao mara hii sikutaka kuupoteza (*BA*, 116). Kutembea juu ya maji inathibitisha sheria za ushirikishi ya binadamu na mazingira kwa mujibu wa Stanley Tambiah. Sheria hii inawezesha binadamu kuhusiana na mazingira moja kwa moja na kukaidi hali halisia ya matendo ya binadamu (Warnes, 2009).

Peter Pan ni mhusika aliyeonyesha sifa zisizo za kawaida. Kwa jina lingine alijulikana kama UMERO-JAPA, jina ambalo kwa maono yangu linamaanisha nchi za Amerika, Uropa na Japani. Peter Pan ametumiwa kama mhusika kumaanisha nchi zilizoendelea na ndiyo sababu kuu ya nchi zinazoendelea kuendelea kuishi kwenye lindi la umaskini. Mhusika huyu alikuwa mrefu kupita kiasi:

18. Nilijitahidi kusimama ili niweze kuliona jitu hilo vizuri. Ilikuwa shida kuliona sawasawa. Miguu yake ilikuwa mikubwa ajabu. Nilirudi nyuma kuweza kuliona vizuri lakini likarefuka nikashindwa kuliona vizuri. (*BA*, 14)

Kutokana na urefu huu alikuwa na uwezo wa kukimbia na kutembea haraka. Urefu huu unaashiria ugumu wa watoto wasichana-wavulana huntha kupatikana katika safari yake ya kuwatafuta. Aidha, alikuwa na uwezo wa kuchipuka na kutoweka ghafla:

19. Bina-Adamu alishtukia amesimama na jitu kubwa, hakuona alipotokea. Fauka ya hayo baada ya kukutana na jitu hili alitoweka kighafla huku akiacha harufu ya beberu. (*BA*, 14)

Uwezo huu unaashiria athari kubwa ya ukoloni katika bara la Afrika. Ukoloni huu umekuwa kikwazo kikubwa katika ustawi wa nchi za Afrika.

Katika riwaya ya *DY,* Kilua, bintiye Ndi- anao uwezo wa kupenya akili na nafsi za wahusika wengine:

20. Uliashiria kumfahamu bila ya kunifahamisha. Ilikuwa kama baina yetu kumeanza kutunga *telephathy:* njia ya kuwasiliana bila kuwasiliana. […]. Kilua ana kipawa cha ajabu cha kuweza kupenya kichwa cha mtu

yeyote ili kujua anafikiri nini na kisha kuwaka umeme wa fikra ulioweza kufika na kumulika upeo wa mbali wa mawazo. Ukitaka la haki, Kilua kilikuwa kitoto halisi na adimu cha wakati wake; cha dunia yao! Dunia ya leo! (*DY*: 91, 92)

Wahusika ambao wanawasiliana kwa njia ya fikra. Hii ni njia ya mawasiliano ya moja kwa moja ya fikra, hisia kutoka mtu moja hadi mwengine bila kutumia maneno, maandishi au njia zozote za kihalisia.

Uhalisiamazingaombwe unajitokeza zaidi kupitia mhusika ambaye ana uwezo wa kupasua kuta:

21. Elena Mejias, katika *Mtoto Mwovu,* ambaye anaweza kupasua kuta, kupenya chumbani mwa mamake na kumkuta na Bernal, mwanamme wa mamake ambaye yeye Elena alimpenda kwa ishara. Aaaa, nani anajali tena na wahusika mviringo? Nani aliyebaki kushikilia uhalisia mkavu? (*DY*, 92)

Katika sehemu hii mhusika Elena Mejia ana uwezo usio wa kawaida; kupasua ukuta. Mhusika huyu anapopasua ukuta anamkuta mamaye na mpenzi wake Bernal. Hii inabainisha mivurugo ya jamii. Inaonekana kuwa mtoto na mwanawe wamekuwa wakimchumbia mwanamme moja. Zaidi ya hayo, Ndi- anaonyeshwa kuwa na uwezo wa kugusa mbingu:

22. Kila usiku, kwa muda wa miezi miwili, nilitoka juu kabisa ya meli kuweza kugusa mbingu. Nilitaka niwe huko kusikiliza bahari katika shwari yake na dhoruba na nguvu zake za mawimbi. (*DY*, 94)

Dondoo hili linatuonyesha Ndi- akigusa mbingu. Kihalisia tendo hili haliwezekani. Kugusa mbingu katika muktadha huu unaashiria hamu ya binadamu kutaka kuzuru dunia kote. Hali hii inatukumbusha Christoper Columbus na Vasco Da Gama waliogundua bara la Amerika na India mtawalia. Ugunduzi huu ulisababisha ukoloni duniani (Rodney, 2015). Aidha, Ndi- anatuonyesha mivurugo ya jamii ilivyokithiri katika jamii. Fauka ya hayo, Ndi- alikuwa na uwezo wa kuona kupitia vizuizi vyovyote:

23. Wakati wote huu nilikuwa nimepoteza sehemu zote za mwili. Ki wapi kidole changu? Zi wapi hisia zangu? Pamoja na kufunikwa gubigubi lakini, niliweza kwa macho ya eksirei, kuona kila nilichotendewa. (*DY*, 182)

Katika sehemu hii, Ndi- anasafishwa na Bi M, Yungi na Bi Juba. Hii ni kama njia ya kusafisha uovu uliokuwa umekithiri katika jamii. Kimazingaombwe anao macho yanayoona kupitia vyombo vilivyozibwa kama ukuta. Aidha, Ndi- ana uwezo wa kuumba binadamu:

24. Wewe uwe nani ila takataka za akili yangu. Nimekuumba mwenyewe uwe mchawi mkondefu kama ng’onda. (*DY*, 86)

Katika dondoo hili, Ndi- anaonyeshwa kuwa ana uwezo wa kumwuumba Bi Mize na kumfanya awe mchawi jambo ambalo linatekelezwa na Mungu pekee. Kwa hivyo Ndi- anaonekana kuwa na sifa ya uungu. Sifa ya uungu inajitokeza zaidi pale Ndi- anapodai kuwa alikuwepo kabla ya Ulimwengu kuumbwa:

25. Nilikuwa sijawahi kuona vua la aina hii maisha yangu yote. Nilikuweko wakati wa vua la Masika la maleleji, nchi hii ilipokuwa ikifinyangwa na Mungu. (*DY*, 165)

Hii ni sifa ya kiungu ambayo inaweza kuhusishwa na Yesu wa Bibilia ya Kikristo. Yesu ni mwanaye Mungu na alikuwa kabla hata dunia kuumbwa kama inavyodhihirika katika kitabu cha Yohanna 1:1-5. Aidha, Ndi- anatuambia kuwa alikuwa na sifa ya kuzuia kufa (*DY*, 211). Kihalisia hakuna binadamu duniani ambaye ana uwezo wa kuzuia kufariki asipokuwa Mungu.

Katika riwaya ya *BAF,* wahusika wengi wamekuwa na sifa zisizo za kawaida. Kwanza ni marafiki wa K:

26. Delpiero alimeza eneo zima la ardhi la pahala fulani tumboni mwake. Wavuvi waliposimama kidete kupuliza cheche zao za uchungu, […] kisha alivuta hewa, mapafuni mwake kuzizima cheche zenyewe kwa pumzi zote alizoweza kuzitoa. (*BAF*, 13)

Delpiero amekuwa rafiki wa dhati wa K kutoka nchi za nje. Alipofika katika bara la Afrika aliwanyanyasa wavuvi kwa kuwakataza kuvua samaki katika Bahari Hindi. Wavuvi walipoteta, kuna uhalisiamazingaombwe ambao ulitokea. Delpiero alimeza hewa yote. Hii inadhihirisha uovu na ukatili wa viongozi. Sawia na hayo Miyazawa amefuga kucha zenye urefu wa meli nzima:

27. Miyazawa […]. Zile gari alizokuja nazo kuziotesha uwanda wa mzogazoga na kuziuza kwa bei kubwa ajabu- ingawa kwao takataka. Waliokuwa karibu naye wanasema kafuga kucha zenye urefu wa meli nzima, na hupita maeneo mbalimbali kunukiliza harufu fulani kama mbwa. Baadaye akigundua kitu, huanza kuchimba kwa kucha zake mwaka mzima mfululizo. Na kila mwenyeji anayepita na kumwona humwuliza, 'Unachimba nini? Na yeye hujibu, 'Dhahabu na almasi' Wenyeji bila ya shaka hucheka na kuridhika na upumbavu wake. (*BAF*, 13)

Uhalisiamazingaombwe wa ufugaji wa kucha sawia na meli inabainisha mivurugo ya jamii. Mivurugo hii ni kupitia ununuzi wa magari kutoka nchi za ng'ambo. Mara nyingi magari haya huwa hayatakikani katika nchi zao. Kwa hivyo bara la Afrika linakuwa kama sehemu ya kurusha zisizohitajika. Aidha, nchi zilizoendelea zinachukuwa raslimali ya nchi zinazoendelea kama dhahabu na almasi. La kushangaza ni kuwa katika nchi hizi raia hawaelewi umuhimu wa madini haya.

Mzuka ni mhusika ambaye utafiti ulibaini alikuwa na sifa zisizo za kawaida kuanzia mwanzo wa riwaya hadi mwisho. Sifa hizo zinaonekana kama zifuatavyo:

sura ya fuvu, (*BAF*, 19), Kichogo cha shingo *kumemetuka,* (*BAF*, 21), kuwa moshimoshi tu; uso wa bango, mfuto; si wa mdomo wala pua, si wa miguu wala mikono-mzuka! (*BAF*, 69). Sifa hizi zilikuwa ni za kuogofya hasa kwa K. K ni mhusika ambaye alikuwa amepita mipaka kutokana na uovu wake. Hii ilikuwa njia pekee ambayo ingeweza kumfikia yeye na kumwadhibu. Kama ilivyotajwa, K alikuwa amewanyanyasa raia wake kuanzia unyakuzi wa ardhi, ufisadi uliokithiri, unyaguzi wa bibi wa watu (kama mkewe Sururu).

Mwishoni mwa riwaya ya *BAF,* Maajuza ni mhusika ambaye ana sifa zisizo za kawaida:

> 28. Wote, watoto na watu wazima, walisita kula kwanza. Wakatazamana na kisha wote walimgeukia Maajuza ambaye katika nuru hafifu ya kibatari alionekana kama zigo kubwa la kuni lililoinamishiwa kitini. (*BAF*, 116)

Maajuza alionekana kama zigo kubwa la kuni. Hii ni sifa isiyo ya kawaida. Maajuza alikuwa nyanya wa K. Katika tamaduni za Kiafrika K alikuwa anafaa kumtunza Maajuza katika umri wa uzeeni. Lakini kutokana na ubinafsi wa K, alimtelekeza. Si Maajuza pekee bali jamii nzima:

> 29. Baadhi walikuwa wakubwa kwake na sasa wameshakonga kabisa kabisa. Miili na vizazi vya wote lakini vilikuwa kama kurasa za vitabu vilivyoashiria maisha yao magumu ya fukara. (*BAF*, 117)

Hii ni mivurugo iliyokithiri katika jamii ya kisasa. Watu hawataki kuwatunza wazazi na jamii zao. Wengi hasa vijana walio na kazi wanaenda na kuishi mijini huko wakiwasahau hata wazazi wao.

Kwa ujumla, wahusika wasio na sifa zisizo za kawaida wametumiwa na waandishi kusawiri mivurugo ya jamii iliyopita mipaka. Wahusika wa kihalisia hawangeweza kutumiwa kwa sababu mivurugo hii ni changamano zaidi. Ili jamii na wasomaji waweze kuona maovu yaliyokithiri katika jamii, wahusika hawa walitumiwa kama njia ya kugusa hisia zao ili waweze kuona uzito wa mivurugo katika jamii ya kisasa na waone haja ya kubadili mienendo yao.

**Hitimisho**

Wahusika ni viumbe muhimu katika kazi yoyote ya fasihi, wahusika hujenga dhamira na maudhui. Katika kazi za kihalisia wahusika wamekuwa ni wale ambao wanawakilisha wahusika wanaopatikana katika jamii. Jamii ya kisasa imejaa mivurugo mingi ambayo wahusika wa kihalisia hawawezi kutumiwa na kuwasilisha ujumbe ufaao kwa wasomaji na jamii kwa ujumla. Wahusika wa kiuhalisiamazingaombwe ni mwafaka katika jamii ya kisasa iliyo na mivurugo mingi na ya kimazingaombwe. Mwandishi ni sharti abuni wahusika ambao watagusa hisia ya msomaji na kumfanya aonye jamii kwa undani. Katika kufanya hivyo, usawiri wa uovu katika jamii utakuwa unafaulishwa. Makala haya yametimiza lengo ambalo linahusu uhakiki wa wahusika wa kiuhalisiamazingaombwe na namna wanavyowasilisha mivurugo ya jamii.

**Marejeleo**

Chanady, A. (1985). *Magical Realism and the Fantastic: Resolved Versus Unresolved Antinomy*. New York: Garland.

Childs, P. na Fowler, R. (2006). *The Routledge Dictionary of Literary Terms*. New York: Routledge.

D'Haen, Theo L. (2005). *Magic Realism and Post Modernism. Decentering Priviledged Centers*. New York: Routledge.

Kegley, W.C. na Raymond, G. (2014*). The Global Future: A Brief Introduction to World Politics*. Boston: Wadsworth Cengage learning.

Khamis, S.A.M. (2008). Nadharia, Ubunifu, Uchambuzi na taaluma ya Kiswahili. Katika: O. Ogechi, N.L. Shitemi na K.I. Simala (wah.). *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Eldoret: Moi University Press.

Mazrui, A, A. (1990). *Cultural Forces in World Politics*. London: James Currey.

Mohamed, S.A. (2006). *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press.

………………. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mriraria, S.E. (2004). Fasihi Simulizi na Teknolojia Mpya. *Swahili 14 (197-206)*

Mwamzandi, I, Y. (2013). Riwaya za Karne ya 21 na Udurusu wa Nadharia za Fasihi. *Swahili Forum 20 (48-66).*

Poncian, J. na Mgaya S. E, (2015). Africa's Leaderhip in the 21st Century: What Can Leaders Learn from Africa's Pre-Colonial Leadership and Governance? *International Journal of Science Studies. Vol. 3, No. 3; May 2015.*

Rettova, A. (2016). From *Mimesis* to *Mize:* Philosophical Implications of Departures from Literary Realism. Katika: C. Vierke, na K. Greven (wah). *Dunia Yao: Utopian/Dystopian in Swahili Fiction.* Cologne*:* Rudiger Koppe Verglag.

Rodney. W. (2015). *How Europe Underdeveloped Africa.* Nairobi: East Africa Publishers Ltd.

Tilak, R. (1993). *History and Principles of Literary Criticism.* New Dehi: Rama Educational Publishers.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Wafula, R. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2008). *Kichocheo cha Fasihi.* Nairobi: Focus Publications Limited.

……………….... (2002). *Bina-Adamu!* Nairobi: Phoenix Publishers.

Warnes, C. (2009). *Magical Realism and postcolonial Novel: Between Faith and Irreverence.* New York: Palgrave Macmillan.